## Kiasi cha mbolea

Kabla ya kuamua aina na kiasi cha mbolea ni vyema kupima afya ya udongo (rutuba) kwenye shamba. Endapo mkulima hajapima afya ya udongo wa shamba lake anashauriwa kutumia viwango vya jumla kwa ekari vilivyopendekezwa kitaifa ambavyo ni;

Kirutubisho cha naitrojeni kwa ekari moja inapaswa kuwa kilo 40(N) sawa na mifuko miwili ya urea. Fosiforasi ni kilo 10(P) na potashi ni kilo 10(K).

## PALIZI.

Magugu huathiri sana zao la mpunga. Athari za magugu kwa zao la mpunga ni pamoja na kushindana na mpunga kwa mwanga, maji na lishe, kupunguza ufanisi wa mbolea ya naitrojeni, magugu hupunguza mavuno, huwa ni maficho ya wadudu na vimelea vya magonjwa. Hakikisha unapalilia vizuri shamba lako

## Aina ya Palizi

- Kung'olea kwa mikono
- Kupalilia kwa mashine na vifaa rahisi mfano, kutumia vipalizi (weeders; rotary na cono weeder
- Tumia viuatilifu (viua-gugu vinavyochagua na visivyochagua aina ya magugu)



Kupalilia kwa kutumia vipalizi vya kusukuma kwa mikono



Kipalizi cha kusukuma kinachotumia mashine



Kipalizi cha kusukuma kwa mikono kisichotumia mashine

## KUVUNA

Shughuli za uvunaji wa mpunga ni pamoja na kukata, kurundika, kupura, kusafisha, na kusafirisha. Ni muhimu kutumia njia nzuri za kuvuna mpunga ili kuweza kuongeza mavuno ya nafaka, na kupunguza uharibifu wa nafaka na kuzorota kwa ubora.

Mwongozo wa uvunaji mzuri wa zao la mpunga :-

- Vuna kwa wakati na kiwango cha unyevu unaofaa (nyama nono), masuke mengi 80% hubadilika rangi kutoka kijani na kuwa njano au kahawia kutegemea aina ya mpunga
- Epuka ucheleweshaji wa kupura baada ya kuvuna
- Safisha/peta nafaka vizuri baada ya kupura
- Kausha vyema (anika) baada ya kupura mpaka kiwango cha asilimia 14 cha unyevu

Mpunga uhifadhiwe vizuri kwenye sehemu isiyo na unyevu, wadudu, na wanyama waharibifu


**Taasisi ya utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)**
Makao Makuu Makutupora,
Barabara ya Arusha,
S.L.P 1571, **DODOMA**
Baruapepe: info@tari.go.tz & dg@tari.go.tz

Kwa maelezo zaidwasiliana na:-
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
**KITUO CHA IFAKARA**
Sanduku la Pekee -Ifakara
Morogoro- Tanzania
Simu :- +255 232 934 156
Nukushi :- +255 232 625 361
Barua pepe: **cmkatrin@tari.go.tz**

Kimetayarishwa na:
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
**KITUO CHA IFAKARA**


TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

TARI
Transforming Agriculture

# KANUNI BORA ZA KILIMO CHA MPUNGA





## UTANGULIZI.

Mpunga ni zao muhimu kwa matumizi ya chakula na hata biashara. Ongezeko endelevu la uzalishaji wa mpunga linahitaji matumizi ya aina bora ya mbegu, mbinu bora za kilimo, mbinu bora za uzalishaji zinazozingatia mabadiliko ya tabia nchi na teknolojia nyinginezo zilizoboreshwa kwenye mnyororo mzima wa thamani.

## MAZINGIRA YA USTAWISHAJI

Mpunga hustawi katika Ikolojia tofauti kulingana na aina ya mbegu.

- Ikolojia ya mabondeni
- Ikolojia ya umwagiliaji
- Ikologia ya miinuko
- Ikolojia ya mashamba yaliyoathiriwa na chumvi na magadi

## UTAYARISHAJI WA SHAMBA

Ili kupata mavuno mengi na mazuri shamba la mpunga lilimwe na kusawazishwa udongo (*leveling).* Hii husaidia mtawanyiko sawa wa maji shambani, mizizi kupata maji na virutubisho vingine kirahisi, huongeza ufanisi wa mbolea kwenye kurutubisha mmea na huleta ukuaji na uwiano sawa wa muda wa kukomaa, mimea pia kudhibiti magugu shambani.

Endapo shamba litakuwa na magugu mengi kabla ya kulimwa unashauriwa kutumia viua gugu (dawa za kuua magugu)

## KUCHAGUA MBEGU BORA ZA KUPANDA

Hakikisha unapata mbegu bora zilizothibitishwa kitaalamu na zinazoendana na ikolojia inayolimwa. Kwa kawaida mbegu bora hupatikana kutoka kwenye vyanzo vya kuaminika kama vile makampuni ya uzalishaji mbegu mfano ASA, Taasisi za utafiti wa kilimo mfano TARI na pia mbegu za daraja la kuazimia (QDS)



## BAADHI YA MBEGU BORA ZA MPUNGA ZILIZOTHIBITISHWA TANZANIA NA IKOLOJIA INAYOFAAA KUPANDWA

| IKOLOJIA | MBEGU |
|---|---|
| Umwagiliaji/ Mabondeni yenye maji ya kutosha | TXD 306 (SARO 5) TXD 88, Komboka, Tai, TARI RIC 1, TARI RIC 2, TARI RIC 3. |
| Mabondeni | TARI RIC 1, Supa, Komboka, Tai |
| Milimani/Miinuko | NERICA 1 *(Baraka),* NERICA 2 (*Tumaini),* NERICA 4 (*Pato*), NERICA 7(*Faraja*), WAB (*Ziada*) |
| Mashamba yaliyoathiriwa na chumvi na magadi | SATO 1, SATO 9 |

## NJIA MBALIMBALI ZA UPANDAJI WA MPUNGA

***a. Kupanda mbegu moja kwa moja shambani***

Mbegu zinaweza kupandwa moja kwa mmoja shambani kwenye mashimo yaliyo kwenye mstari au pasipo kufuata mstari (kumwaga). Hata hivyo inapendekezwa kupanda kwa mstari kwa vile ina faida nyingi mfano kurahisisha palizi

Kupanda moja kwa moja kwenye mistari kunaweza kutumia vijembe au kutumia mashine (planters)

***b. Kupanda kwa kutumia miche***

♦ ***Kuandaa kitalu***

Mbegu hupandwa kwanza kwenye kitalu kabla ya kupandikizwa miche shambani.

i. Andaa tuta la kitalu cha mbegu lenye upana wa meta 1-1.5 na urefu unaofaa kulingana na eneo lakini usioleta kero wakati wa kuhudumia

ii. Pandisha udongo kiasi cha urefu wa sentimeta 5-10

iii. Tengeneza njia ya kuingizi maji na mifereji ya kutolea maji

iv. Ruhusu maji kuingia kwenye kitalu (kifanye kiwe kimetota maji)

v. Sia mbegu zilizoatamishwa na kuanza kumea kwa kiasi cha gramu 100 kwa kila meta moja ya mraba

♦ **Kupanda miche shambani**

Shamba la kupandikiza miche linatakiwa liwe limelimwa na kuchavangwa vizuri

⇒ Miche ya kupandikiza inatakiwa iwe na umri wa siku 21(au siku 8-14 kwa kilimo shadidi)

⇒ Nafasi inayopendekezwa ni sentimeta 20 kati ya mashina na sentimeta 20 kati ya mistari. (wakati mwingine sentimeta 25 kwa 25 au 15 kwa 30 zinashauriwa kwa madhumuni mbali mbali)

⇒ Pandikiza miche 2-3 kwa shina

⇒ Panda miche kwa mistari kama inavyo onekana kwenye picha



## UWEKAJI WA MBOLEA

Virutubisho muhimu kwenye zao la mpunga ni naitrojeni (N), fosiforasi (P) na potasiamu (K). Pia virutubisho vya salfa, zinki, na boroni vinatakiwa japo kwa kiasi kidogo

Wakati muafaka wa kuweka mbolea na matokeo yake;

***Mbolea ya kupandia***

Huwekwa wakati wa kuchavanga au wakati wa kupandikiza -DAP, NPK, TSP au Minjingu

- Zinasadia kutoa mizizi imara
- Zinasaidia kuongeza idadi ya pacha

***Mbolea ya kukuzia***

Inashauriwa kuwekwa mara mbili (asilimia 70 iwekwe wakati wa kupacha na asilimia 30 iwekwe wakati wa mimba dume(kuzaa))

i. Wakati wa kupacha (siku 14 baada ya kupandikiza) Urea, SA au CAN

- Zinasaidia kuongeza idadi ya pacha

ii. Wakati wa mimba dume (siku 25 kabla ya kuchanua) –Urea, SA

- Inasaidia ujazaji wa punje na uzito